# Mwongozo wa Wazazi wa Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza

HISD | Multilingual Education
MEETING DIVERSE NEEDS. CREATING OPPORTUNITIES.

Ikifanya kazi chini ya miongozo ya Wakala wa Elimu wa Texas, HISD ina programu za maelezo zilizobuniwa kwa mahitaji na matakwa maalum ya kila mwanafunzi. Matoleo yanajumuisha uongozi wa usimamizi na usaidizi kwa Lugha Mbili na Kiingereza kama elimu ya Lugha ya Pili na programu mbadala za lugha kwa wanafunzi wote waliotambuliwa kama Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELL) au mhamiaji, mhamiaji wa kazi, mkimbizi, na wanafunzi wageni.

Ili uhakikishe kwamba wanafanuzi hawa wanahitimu kutoka shule ya upili kwa mafanikio na wako tayari kuhudhuria chaguo ya baada ya shule ya elimu wanayotaka, mifumo kamili na ya utendaji y upangaji na utiifu imetaasisishwa.

## MODELI ZA PROGRAMU

Kwa wanafunzi wa shule ya msingi, kwa sasa wilaya inatoa Programu za Mpito za Lugha Mbili za Kihispania, Programu ya Urithi wa Kitamaduni wa Lugha Mbili (Kivietinamu), Mafunzo ya Kichina cha Mandarini, Mafunzo ya Kiarabu, na Programu ya Mafunzo ya Kifaransa pamoja na Kiingereza kama programu za Lugha ya Pili (ESL) kwa watu wanaozungumza lugha zingine.

Shule za upili zinatoa ESL/Programu za Elimu ya Kiingereza ya Maelekezo na Maudhui ya Maelekezo kwa ELL katika madarasa ya 6-12. Programu za lugha mbili pia zinatolewa katika shule teule za Lugha Mbili.

## UFAFANUZI WA PROGRAMU ZA LUGHA

- Lugha Mbili za Mpito: Huwahudumia wanafunzi wanaozungumza Kihispania waliobanishwa kama wenye upungufu wa ustadi wa Kiingereza, na huwahamisha wanafunzi kwenye maelekezo ya Kiingereza pekee. Muundo huu hutoa maelekezo katika maeneo ya maudhui ya kujua kusoma na kuandika na kielimu kupitia mtindo wa lugha ya kwanza ya mwanafunzi, pamoja na maendeleo ya lugha ya Kiingereza.




- Lugha Mbili: Ni programu ya nyongeza ya lugha mbili kwa wanafunzi wanaozungumza Kihispania na programu ya mafunzo ya lugha ya kigeni kwa wanafunzi wanaozungumza Kiingereza. Katika madarasa ya Njia Mbili, mchanganyiko wa wazungumzaji wa asili wa Kihispania na wazungumzaji asili wa Kiingereza wanafunzwa pamoja kwa juhudi za kukuza uwezo kamili wa kuzungumza lugha mbili na uwezo wa kusoma na kuandika kwa lugha zote mbili kwa makundi hayo mawili ya wanafunzi.

Katika kiwango cha shule ya upili (Shule ya Kati/Shule ya Upili), wanafunzi wanaoshiriki katika programu kwa kawaida huchukua madarasa mawili-matatu kwa lugha ya Kihispania.

Maelezo ya kupanga katika Shule ya Msingi na Shule ya Upili.

- Urithi wa Utamaduni: Wazungumzaji wa Kivietinamu, waliobainishwa kama ELL, hupokea usaidizi wa lugha msingi kwa uendelezaji wa uwezo wa kusoma na kuandika/dhana huku wakijifunza Kiingereza katika mpangilio wa kimaelezo wa ESL.

Programu hii inatolewa katika Shule ya Msingi ya Park Place peke yake.

- ESL: Imebuniwa kwa wanafunzi kufunzwa kwa lugha ya Kiingereza peke yake. Walimu hutumia mbinu za ESL katika kila mada ili kufanya maudhui rahisi kueleweka.

Katika programu ya ESL ya **shule ya upili**, kozi za sanaa za lugha ya Kiingereza za "maelekezo" zinajumuishwa kukuza ustadi wa kuelewa, kuzungumza, kusoma, na kuandika. Wakishatambuliwa kama ELL, wanafunzi wanawekwa katika madarasa ya Kiingereza yanayofaa kulingana na kiwango chao.

## PROGRAMU YA WAGENI

Programu ya wageni ni mtazamo wa upangaji ESL uliobuniwa hasa kuhudumia na kuelimisha wanafunzi wageni wasiozungumza Kiingereza. Programu ya wageni husaidia wanafunzi wahamiaji kuzoea nchi, lugha, na shule yao mpya. Programu hii hutoa usaidizi wa kimaelezo wa lugha kwa wanafunzi, kulingana na kiwango chao cha ustadi wa lugha ya Kiingereza, kupitia kozi za Ukuzaji wa Lugha ya Kiingereza, kozi za maudhui ya kimaelezo kwa kutumia mbinu ya ESL, na kozi za kusoma za ESL.

Kampasi za shule za upili zimepangwa kama KITOVU, Za Kipekee au Shule za Uhamishaji kwa Wageni. Ikiwa mtoto wako yupo katika Shule ya Uhamishaji na ungependa apokee programu ya Wageni bonyeza hapa.

Huu ni uwekaji wa hiari.

## PROGRAMU YA ELIMU YA MHAMIAJI WA KAZI

Lengo la Programu ya Elimu ya Mhamiaji wa Kazi (MEP) ni kubuni programu zinazowasaidia wanafunzi wote wahamiaji wa kazi kukabiliana na mabadiliko ya kielimu, changamoto za usafiri, vikwazo vya kitamaduni na lugha, ubaguzi wa kijamii, matatizo mbalimbali ya kiafya na mambo mengine yanayohusiana na mtindo wa maisha wa uhamaji ili kufaulu shuleni na kuvuka kwa elimu au ajira ya baada ya elimu ya shule ya upili kwa mafanikio.

- Angalia orodha ya mahitaji ya kustahiki hapa
- Tazama programu ya brosha ya Mhamiaji wa Kazi
- Pakua Utafiti wa Familia kwa lugha ya Kiingereza/Kihispania, Kivietinamu au Kiarabu.

## PROGRAMU YA SHULE YA MAJIRA YA JOTO



HISD hutoa shule ya majira ya joto kwa ELL waliosajiliwa katika PK na K wakati wa mwaka wa shule (na watakaoingia K au darasa la kwanza katika majira ya majani kupukutika). Programu hii ni nyongeza ya mwaka wa shule na itafunzwa na walimu waliohitimu wa Lugha Mbili/ESL. Maelekezo haya yanalenga ukuzaji wa lugha na Ufahamu na Ujuzi Muhimu wa Texas unaofaa kulingana na darasa (TEKS).

Ili upate maelezo zaidi kuhusu kustahiki kwa mwanafunzi kuhudhuria shule ya majira ya joto tafadhali wasiliana na shule ya mtoto wako au bofya hapa.

## KUHUDHURIA NA KUJIANDIKISHA KATIKA SHULE

HISD hukuza dhana ya shule za mtaani na ushiriki wa jamii. Kila shule katika wilaya inahudumia mtaa fulani ndani ya kanda ya mahudhurio ya shule hiyo, na kila mwanafunzi aliyesajiliwa katika programu ya elimu ya kawaida anapangwa kwenye shule fulani kulingana na mahali wazazi wake au walezi wake wa kisheria wanaisha.



Ili ujue ni shule gani zinazohudumia makazi yako, tafadhali bonyeza kwenye Chagua Shule au piga simu kwa Idara ya Uhamishaji wa Wanafunzi kupitia 713-556-6734. Kwa maelezo zaidi, unaweza pia:

- Kutazama orodha ya Kampasi za Lugha Mbili
- Pakua Ramani ya Lugha Mbili
- Tazama ramani za mipaka ya shule.

Kwa maelezo zaidi nenda kwenye Chaguo ya Shule.

## RASILIMALI ZA JAMII

Idara ya Kuhusisha Familia na Jamii ya wilaya imeunda mkusanyiko wa rasilimali zinazoweza kukunufaisha wewe na familia yako:

- Pitia orodha ya wasifu wa shirika ili upate maelezo zaidi kuhusu huduma za ESL na GED za watu wazima hapa.
- Tazama miongozo zaidi pamoja na programu za baada ya shule, kambi za majira ya joto, vituo vya kijamii, ujuzi wa kutumia kompyuta, uelewaji wa

utamaduni, elimu ya familia, uelewaji wa STEM, ufasiri, mafunzo, na ushauri kwa vijana. www.houstonisd.org/communityresource

- Programu ya Hipi: Huwafunza wazazi wa watoto wenye umri wa miaka mitatu na minne shughuli za kimaelezo zinazopendekeza mafunzo na maendeleo ambayo wanaweza kufanya mazoezi na watoto wao baadaye.

## WASILIANA NASI

HISD Multilingual Education
MEETING DIVERSE NEEDS. CREATING OPPORTUNITIES.

Kwa maelezo zaidi kuhusu programu hizi wasiliana na Idara ya Programu ya Lugha Nyingi kupitia 713-556-6961 au tembelea tovuti yetu.